



# **Viwango vya Kilimohai Afrika Mashariki**

## **Uzalishaji wa Mifugo**



***Imeandaliwa na Shirika la Kilimohai Tanzania- TOAM,  
2026***



In cooperation with



# 1 Asili ya Wanyama

EAOPS: Sehemu ya 7.1

**Je, ni wanyama gani wanaruhusiwa katika kilimohai?**

- Tumia wanyama waliozaliwa na kulelewa kwa mfumo wa kilimohai inapowezekana.
- Ikiwa hawapatikani wanyama wadogo wasio wa kilimohai wanaweza kutumika, lakini lazima wapitie kipindi cha mpito kabla bidhaa zao (maziwa, nyama, mayai) kuuzwa kama za kilimohai

## 2 Kipindi cha Mpito

EAOPS: Sehemu ya 7.1



Ng'ombe: Kwa uzalishaji wa nyama **Miezi 12**



Sungura wa nyama: **siku 45**



Kuku wa nyama: **siku 45**



Mbuzi, kondoo na nguruwe kwa uzalishaji wa nyama: **miezi 3**

- Uzalishaji wa maziwa kwa aina zote mifugo **miezi 3**
- Uzalishaji wa mayai kwa aina zote **siku 42**

# 3 Makazi ya wanyama

## EAOPS: Sehemu ya 7.3

- Wanyama wanapaswa kuishi katika mazingira gani?
- Mazingira safi, salama na yenye nafasi ya kutosha
- Tumia vifaa vya asili kama mbao, matofali, majani makavu
- Wape hewa safi, mwanga wa asili, kivuli, nafasi ya kutembea, kulala na kula kwa uhuru
- Hairuhusiwi kuwafungia wanyama kwenye sehemu ndogo na kusababisha msongamano.
- Linda wanyama dhidi ya jua, mvua, upepo na wanyama wakali



## 4 Lishe na Ulishaji

### EAOPS: Sehemu ya 7.6

- Wanyama wanapaswa kula chakula cha kilimohai.
- Hadi asilimia 40 ya chakula kisicho cha kilimohai kinaweza kutumika endapo cha kilimohai hakitoshi
- Zaidi ya asilimia 50 ya chakula itoke shambani humo au maeneo ya karibu ya malisho



- Hairuhusiwi chakula cha kemikali, vichocheo vya ukuaji au vihifadhi vya kemikali
- Damu au samadi hairuhusiwi kwenye chakula au chakula kilichotibiwa kwa kemikali
- Vitamini na madini ya viwandani yasiyozidi 5% yanaweza kutumika pale vya asili havitoshi
- Wanyama wanaocheua wanapaswa kuchungwa mara kwa mara, kupata malisho ya nyasi na nyuzinyuzi/roughage

# 5 Afya ya Wanyama

## EAOPS: Sehemu ya 7.7



Vipi kama dawa za asili hazikuwa na ufanisi au hazipatikani katika eneo langu? na vipi kuhusu matumizi ya chanjo je yanaruhusiwa?



Tumia tiba za asili inapowezekana. Kama hazipatikani au hazina ufanisi unaweza kutumia dawa za kawaida au antibiotics chini ya usimamizi wa daktari wa mifugo na kama suluhu ya mwisho. Lakini ni lazima:

- Uweke kumbukumbu za tiba zilizotumika kwanza kuonesha kuwa za asili hazikuwa na ufanisi au hazipatikani
- Kufuata muda maalum uliowekwa kabla ya kuuza bidhaa za mnyama tangu alipotumia dawa (angalau mara mbili ya muda uliowekwa kitabibu (si chini ya siku 14)).
- Kuhakikisha Mnyama asipewe matibabu ya kemikali zaidi ya mara 3 kwa miezi 12 (au mara moja tu kama mzunguko wake wa maisha ni chini ya mwaka mmoja).




**Chanjo zinaruhusiwa pale ambapo magonjwa hayawezi kudhibitiwa kwa njia nyingine au zinapotakiwa kisheria**

# 6

## Usafirishaji na Uchinjaji

EAOPS: Section 7.8



Washughulikie wanyama wa upole na kujali



Wape chakula na maji



Wape alama ya utambulisho



Usitumie vichocheo vya kemikali kabla au wakati wa usafirishaji




Usiwasafirishe zaidi ya masaa 8 bila sababu ya msingi. Usiwaweke juani muda mrefu




Usichanganye wanyama hai na waliokufa

# 7 Mbinu nyingine muhimu za ufugaji



- Watoto wa wanyama wanyonge maziwa ya mama kwa muda unaofaa

- Kamba za kufungia ziwe ndefu kuruhusu mnyama kutembea
- Wape chakula cha ziada wakati wa ukame
- Usikate sehemu za mwili wa mnyama isipokuwa kuhasi, kuweka ringi puani na kuondoa pembe kwa wanyama wadogo tu.



- Wanyama wachungwe au watolewe nje kila siku kuruhusu ya kuonesha tabia ya asili
- Epuka kuwapa msongo wa mawazo utakanao na njaa, kiu, hofu, na maumivu.

- Weka kumbukumbu za za chakula, matibabu na kuzaliwa. Itasaidiwa wakati wa uthibitishaji
- Kusanya samadi kwa ajili ya matumizi ya mbolea
- Safisha banda mara kwa mara.
- Watenge wanyama wagonjwa
- Wanyama wawe huru dhidi ya maumivu, majeraha na magonjwa

## Kuhusu kipeperushi hiki

Kipeperushi hiki kinaonesha mahitaji ya msingi ya viwango vya bidhaa za kilimohai vya Afrika Mashariki vijulikanavyo kama East Africa Organic Products Standards (EAOPS). Kiwango hiki kilipitishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2007 na kufanyiwa maboresho kila baada ya miaka mitano hivyo kuwa kiwango rasmi kwa Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi.

Kipeperushi hiki rahisi kimeandaliwa na Mwamvuli wa Kilimohai Tanzania (Tanzania Organic Agriculture Movement -TOAM) kupitia Mradi wa Kitovu cha Maarifa ya Kilimo Ikolojia Hai Afrika Mashariki (Knowledge Hub for Organic Agriculture and Agroecology in East Africa – KHEA).

Mradi huu unalenga kuandaa, usambazaji wa maarifa na matumizi ya kilimo Ikolojia hai katika Afrika Mashariki. Unafadhiliwa na GIZ kupitia Biovision African Trust (BvAT)

Unaweza kupata maarifa kama haya na mengine mengi kutoka Tanzania na afrika kwa ujumla kwa kutembelea tovuti: <https://khea-africa.org/> na <https://kcoa-africa.org/>  
KHEA Website

## Mawasiliano

 [info@kilimohai.org](mailto:info@kilimohai.org)

 +255 744 134 999

- Uzalishaji wa Mazao
- Uchakataji wa Bidhaa za kilimohai
- Uzalishaji wa Viumbe Maji
- Ufugaji wa Nyuki